

## KCPE Insha samples 1 pdf

Mfano wa insha ya mdokezo

Moto Shulenii

Nilipokuwa darasani, niliona moshi mwingi ukifuka kutoka chumba cha walimu. "Mwalimu kuna moshi mwingi unaofuka kwenye chumba cha walimu" Nikamwambia mwalimu Kamau aliyekuwa anatufunza somo la hesabu.

Kwa upesi Mwalimu alichungulia dirishani na haraka haraka akaufungua mlango wa darasa. Sote tulimfuata nyuma na tulipokaribia kwenye chumba cha walimu, tayari mwalimu wetu alikuwa amewajulisha walimu wengine kuhusu moto uliokuwa unatambaa kwa upesi. Waama penye moshi pana moto.

Wanafunzi wote walismama uwanjani huku kila mmoja akistaajabu. Kwa kweli chambilecho wahenga ukistaajabu ya musa utaona ya firauni. Bila kusita mwalimu Mkuu alibofya vifute vyta rununu yake nambari 999 ili kuwaita wazimamoto na baada ya dakika tano, Lori lao kubwa lilifika huku vimulimuli vyake vikitoa ishara ya hatari kwa sauti ya juu mno.

Nyuma ya lori, mlikuwa na ambulensi. Mwalimu mkuu alimsalimu dereva na kumfahamisha ya kuwa hakuna mtu ye yote alikuwa amejeruhiwa. Ghafla bin vuu dereva wa ambulensi aliipendua gari na kwenda. Wazimamoto na walimu walijaribu kuuzima moto lakini badala ya kuzimika, uliendelea kurindima kwa nguvu. Wanafunzi wachache walikubalistwa kushirikiana na walimu pamoja na wazima moto. Kwa kuwa umoja ni nguvu na utengano udhaifu, ushirikiano wetu ulituwezesha kuuzima moto baada ya nusu saa.

"Mna bahati sana kwani moto haukuenea kwenye madarasa yenu." Mzimamoto mmoja alisema. "Moto ulianzaje?" Mzima moto mwingine aksauliza. "Hakuna anayejua kiini cha moto wenye." Mwalimu mkuu alijibu.

Baada ya wazimamoto kwenda, mwalimu mkuu alituaambia twende paredi ili kujulishwa mpangilio wa majukumu yaliyo baki.